**UNAWEZA KUSIKIA SAUTI YA MUNGU!**

Katika kipindi hiki cha karne ya ishirini na moja, binadamu wengi wamejitosa kwenye mfumo wa imani unaoabudu yale yanayothibitishwa kwa macho, yenye mantiki au taamuli ya kisayansi kiasi kwamba tunacheka au kuona ajabu mtu atakapodai kuwa anaweza kusikia sauti ya Mungu.

Lakini, sisi hatucheki, kwa sababu zifuatazo. Kwanza, wanawake na wanaume katika Biblia walisikia sauti ya Mungu. Pia, kuna wanawake na wanaume mashuhuri na wanaofahamika leo wanaoshuhudia kuwa wanasikia sauti ya Mungu. Hatimaye, sisi tuna hamu kubwa sana ndani yetu ya kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu, na kumsikia Mungu akizungumza ndani ya mioyo yetu.

Kama Mkristu aliyeokoka, nilihangaika kwa miaka kadhaa kusikii sauti ya Mungu. Nilisali, nilifunga, na nikasoma Biblia yangu na kusikiliza kwa makini sauti hii ndani yangu, bila mafanikio yoyote. Sikusikia sauti yoyote ndani yami! Halafu Mungu akaniweka kando kwa muda wa mwaka mmoja kusoma, kutafakari na kufanya majaribio ya kusikia sauti Yake. Katiki kipindi hiki, Mungu alinifundisha kwamba kuna funguo nne zinazofungua mlango wa sala zinazosikika na kujibiwa na Mungu. Funguo hizi zimenisaidia mimi pamoja na maelfu ya waumini waliojifunza jinsi ya kuzitumia kuingia katika uhusiano wa karibu na Mungu na kubadilisha maisha yao kabisa. Wewe pia unaweza kunufaika na haya utakapomtafuta Mungu kwa kutumia funguo nne zifuatazo. Funguo zote hizi zinapatikana katika kitabu cha Habakuki 2:1-2. Ninakusihi usome mistari hii kabla ya kuendelea.

**Ufunguo # 1: Sauti ya Mungu inasikika katika mioyo yetu kama mbubujiko wa mawazo ya papohapo.**

Biblia inasema kuwa ‘Mungu alinijibu akasema…’ (Hab. 2:2). Habakuki alifahamu sauti ya Mungu. Eliya aliifafanua kama sauti ndogo tulivu (1 Fal. 19:12) inayosikika, na kweli Mungu huzungumza hivi. Hata hivyo, nimeona kwamba kwa wengi wetu, sauti ya Mungu mara nyingi hutujia kama fikra, wazo, picha au hisia za papohapo. Je, haujawahi kujiwa na wazo la kumsalia mtu fulani angali unaendesha gari au kufanya shughuli zako? Swali langu kwako ni, “Uliisikiaje sauti ya Mungu? Je, ilikuwa ni sauti uliyoweza kusikia kwa nguvu au ilikuwa wazo au sauti kimya ya papohapo iliyoangaza mawazo yako?”. Wengi wenu siajabu mtasema kwamba sauti ya Mungu ilikujia kama wazo au sauti kimya ya papohapo.

Kwa hiyo nikajiwazia, “Labda ninaposikilizia sauti ya Mungu, nisikilizie mtiririko wa mawazo ya papohapo. Labda, mawasiliano ya kiroho yanapokelewa kama mawazo, picha na hisia za papohapo”. Kupitia majaribio yangu na maoni rejea kutoka maelfu ya wengine, nimedhihirisha ukweli huu.

Biblia inasadikisha ukweli huu katika njia tofauti. Tafsiri ya ‘paga’, neno la Kiyahudi linaloomaanisha sala za maoembezi, ni “mkutano wa bahati au makutano

usiyoyategemea". Mungu anapotuwekea sala za maombezi kwa ajili ya watu fulani, hufanya hivi kupitia wazo la papohapo usilolitegemea, akiingilia mpangilio wa mawazo yetu. Hivyo, ninapofungua mawazo yangu kwa Mungu, ninasikilizia mtiririko wa mawazo ya papohapo. Nimegundua kuwa mtiririko wa mawazo ya papohapo yanayonijia ninapokaa kwa utilivu kabla ya Mungu ni kwa uhakika kutoka Kwake.

**Ufunguo # 2: Lazima nijifunze kutuliza mawazo na hisia zangu, ili niweze kusikia mtiririko wa mawazo na hisia za Mungu ndani yami.**

Habakuki alisema, "Nitasimama kwenye lindo langu na kujiweka kwenye ngome…" (Hab. 2:1). Habakuki alifahamu kwamba ilimbidi aende sehemu kimya yenye utulivu ili kutuliza mawazo na hisia zake, na kusubiria mtiririko wa mawazo ya Mungu – ambayo yangemjia kwa utulivu moyoni mwake. Zab. 46:10 inatuhimiza tuwe watulivu, ili tufahamu kuwa Yeye ni Mungu. Kila mmoja wetu anaweza kupata ufahamu wa ndani kabisa wa kiroho tunapotuliza akili na viwiliwili vyetu.

Nimegundua njia rahisi kadhaa za kujituliza ili niweze kupokea mtiririko wa Mungu wa papohapo. Njia mojawapo inayonisaidia kutuliza akili yangu ni kumsifu Mungu kwa kumwimbia nyimbo za kumuabudu (tazama Fal. 3:15). Ni pale ninapotulia (kimawazo, kihiari na kihisia) mbele ya Mungu, ndipo mtiririko takatifu unaponijia. Hivyo, baada ya kumuabudu kwa ukimya na utulivu, ninajifungua kupokea mtiririko wa papohapo. Ninapojiwa na mawazo ya mambo niliyoyasahau kufanya, ninayaandika na kuyaweka kando. Iwapo dhamira ya hatia au kutokuwa na thamani inanijia, natubu kikamilifu, halafu najikosha na damu ya Kondoo, najitwisha joho Lake la uadilifu, nikijiona kama asiye na doa mbele Yake (Isa. 61:10; Kol. 1:22).

Kadri ninavyomkazia macho Yesu (Ebr. 12:2) nikiwa mkimya mbele yake, nikimshirikisha katika yale yaliyo moyoni mwangu, ndivyo mazungumzo ya pande mbili yanapotokea. Mawazo ya papohapo kutoka kiti cha enzi cha Mungu yananijia, na hujikuta nikiwasiliana na Mfalme wa Wafalme.

Ni muhimu sana utulie na uwe makini ili uweze kupokea neno halisi la Mungu. Kama hujatulia, utapokea tu mawazo yako. Kama hujamkazia macho Mungu sawasawa, utapokea mtiririko usio halisi, kwasababu mtiririko wa mawazo wa kipawa cha kujua bila kufikiri huibuka kutoka kile ulichokikazia macho. Hivyo, kama utamkazia macho Yesu, mtiririko huu utatoka kwa Yesu. Ukikaza jicho lako kwenye tamaa za moyo wako, mtiririko huu utaibuka kutoka tamaa hizo. Ili upate mtiririko halisi kutoka Mungu, lazima kwanza utulie, na pili, umkazie macho Yesu. Nitarudia, kumuabudu Mfalme kimyakimya, halafu kupokea neno lake katika utulivu huu ni rahisi kutekeleza.

**Ufunguo # 3: Ninaposali, nakaza jicho la roho yangu kwa Yesu, nikiona ndani ya roho yangu ndoto na mawazo mbali ya Mwenyezi Mungu.**

Tumeshagusia mambo hayo katika aya za nyuma; hata hivyo, lazima tuangalie kwa umakini zaidi. Habakuki alisema, "Nitakaa macho nione…", na Mungu alisema, "Andika utakayoyaona" (Hab. 2:1-2). Inavutia kuona kuwa Habakuki aliposali alitarajia kupokea picha kutoka Mungu. Alijitayarisha kufungua macho ya moyoni, kutazama ndani ya ulimwengu wa kiroho ili kuona yale ambayo Mungu alitaka kumuonyesha. Hili ni wazo la kufurahisha.

Sikuwahi kufikiria kufungua macho ya moyoni na kutarajia picha ya Mungu. Lakini, kadri nilivyoliwaza, ndivyo nilivyogundua kuwa Mungu alitarajia nifanye hivi. Alinipa macho ndani ya moyo wangu. Yanapaswa kutumika katika ulimwengu wa kiroho kuona mienendo na mawazo ya mbali ya Mungu. Ninaamini kwamba kuna dunia ya kiroho inayoendelea sambamba nami. Dunia hii imejaa malaika, shetani, roho mtakatifu na Mungu aliyepo kila mahali kila wakati, na Mwana wa Mungu, Yesu, aliyepo kila wakati kila mahali. Hakuna sababu ya kutokuona yote haya, kasoro kwa imani yangu ya mawazo mantiki, inayonishawishi kutoamini na isiyonifundisha jinsi ya kujifungua kuona dunia ya kiroho.

Ili tuone ni lazima tutizame. Danieli alikuwa akiangalia picha katika akili yake akasema, "Nilikuwa natazama… niliendelea kutazama… niliendelea kutazama" (Dan. 7:2, 9, 13). Sasa ninaposali, namtafuta Yesu ndani yami, halafu namtazama huku akizungumza nami, akitenda na kunena yale yaliyo moyoni mwake. Yesu ni Imanueli, Yesu Yu Nasi (Mat. 1:23). Ndivyo hivyo. Utaona mtiririko wa picha za papohapo kama vile unavyopokea mawazo ya papohapo. Unaweza kumuona Yesu nawe katika sehemu ya starehe au ya utulivu kwasababu Yesu yupo nawe katika sehemu starehe au tulivu. Tena, utagundua kwamba picha za kiroho zinakujia kwa urahisi sana kana kwamba utakuwa na tabia ya kuitia kando, ukifikiri kwamba ni wewe na siyo Mungu. (Shaka ni silaha kali ya Shetani dhidi ya Kanisa). Lakini, uking'ang'ania kuandika picha hizi, imani itashinda mashaka yako kadri utakavyogundua kuwa yaliyomo yalizalishwa na Mwenyezi Mungu.

Mungu alijitambulisha kwa watu wa agano lake kupitia ndoto na picha. Alifanya hivi kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo na alisema kwamba, tangia siku Roho Mtakatifu ilimwagika katika Matendo 2, tutegemee kupokea mtiririko endelevu wa ndoto na picha (Mdo. 2:1-4, 17). Yesu, mfano wetu Kamili, alidhihirisha haya kwa kuishi maisha yake yote katika uhusiano wa karibu na Mwenyezi Mungu. Alisema kuwa Hakufanya jambo lolote kwa hiari yake, bali kile tu alichokiona Baba yake akitenda au alichokisikia Baba yake akinenena (Yoh. 5: 19, 20, 30). Je, hii siyo njia ajabu na ya muujiza kuishi!

Je, tunaweza kuishi kutokana na uamuzi wa kiroho kama Yesu alivyoishi? Nia kuu ya kifo cha Yesu na ufufuo Wake ni kuchana shela kutoka juu hadi chini, akitupa njia ya kuingia moja kwa moja katika nafasi ya Mungu, na tunaamrishwa kumkaribia (Lk. 23:45; Ebr. 10:19-22). Hivyo, hata kama ninayoeleza yanaonekana ya ajabu kidogo katika utamaduni wa sasa wa fikra mantiki, imedhirihirishwa na kufafanuliwa kama fundisho kuu la Biblia. Ni muda sasa kurejesha kanisani kilicho cha Kanisa.

Watu wengine watahitaji msaada mkubwa zaidi kuelewa ukweli huu kwa sababu ya tegemezi lao kubwa zaidi katika fikra na tamaduni mantiki. Watapata msaada huu katika kitabu kiitwacho "Ushirika na Mungu (Communion with God)", kilichoandikwa na waandishi hawa.

**Ufunguo # 4: Uandishi, kuandikia sala zetu na majibu ya Mungu, kunatuletea uhuru mpya wa kuisikia na kuiamini sauti ya Mungu.**

Mungu alimwambia Habakuki aandike picha aliyoiona halafu aichonge kwenya mabamba ya taarifa… (Hab. 2:2). Sikuwahi kuwaza kuandika sala zangu na majibu ya Mungu kama Habakkuki alivyofanya alipoamriwa na Mungu. Utakapoanza kutizama maandishi takatifu ya Mungu, utapata sura nyingi zinazodhihirisha wazo hili (Zaburi, Manabii, Ufunuo). Sasa kwa nini sikuwahi kupata wazo hili kabla ya hapo?

Utaratibu huu wa kunakili nilikuja kuuita 'Unukuu', na nikaanza majaribio ya kunukuu. Nilikuja kugundua kuwa utaratibu huu ulinisaidia sana kuona kwa wazi mtiririko wa papohapo wa Mungu, kwa sababu kadri nilivyonukuu niliweza kuandika kwa imani kwa kipindi kirefu cha muda, kwa kuamini tu kwamba ni Mungu. Sikuhitaji kufanya majaribio kadri nilivyopokea mtiririko huu (kwani ingenizuia kuendelea kupokea), kwa sababu nilijua mtiririko utakapokwisha nitaweza kurudi kwenye maandishi yangu na kuyatafakari kwa makini, kuhakikisha kwamba ni sambamba na Maandishi Takatifu.

Utashangazwa utakapojaribu kunukuu. Mashaka yanaweza kukujia mwanzoni, lakini yatupe pembeni, ukijikumbusha kwamba unukuu ni dhana ya kibiblia, na kwamba Mungu yupo, na anazungumza na watoto Wake. Usijitilie maanani sana. Ukifanya hivyo, utakakamaa na kuingilia mwenendo wa Roho Mtakatifu. Ni pale tu tutakapopumzisha akili zetu na kuingia katika mapumziko ya Bwana ndipo Mungu atakapoweza kutiririka ndani yetu (Ebr. 4:10). Kwa hiyo, vaa tabasamu, kaa na utulie kwa starehe, toa karatasi na kalamu yako, na geuza mawazo yako kwa Mungu ukimsifu na kumuabudu, ukitafuta sura Yake. Unapoandika swali kwa Mungu, tulia, kaza jicho lako kwa Yesu, Aliye nawe, na papohapo utakuwa na wazo zuri linalojibu swali lako. Usitilie shaka, lakini uliandike tu. Baadaye, unaposoma maandishi yako, wewe pia utabarikiwa kugundua kuwa kweli unawasiliana na Mungu.

Ujumbe wa mwisho: Usijaribu kunukuu kabla ya kusoma angalau Agano Jipya (vizuri zaidi kama umesoma Biblia nzima), na usijaribu pia kasoro kama umejinyenyekea kwa utiifu chini ya uongozi wa kiroho. Mawazo yanayokuhimiza kubadilisha jambo (au mambo makubwa) yawasilishwe kabla ya kutekelezwa.

Kwa mafunzo kamilifu katika mada hii, agiza Kielelezo cha Masomo cha 'Ushirika na Mungu (Communion with God)' katika tovuti ifuatayo: www.CWGministries.org au piga simu Marekani: 716 652 6990. Tovuti hii pia ina katalogi ya vitabu 50 vilivyoandikwa na Mark na Patti Virkler pamoja na kozi 100 za chuo. Barua pepe: cwg@cwgministries.org.